

Maandishi ya Video ya Kurudi Masomoni

Habari! Mimi ni Dkt. Robert Kobylski, Superintendent wa Davenport Community School District.

Zaidi wa wanamemba 100 wa timu ya Davenport Community School District wamekuwa wakijitahidi kwa wiki kadhaa zilizopita kutengeneza na kuwasilisha mpango wetu wa kurudi masomoni.

Kila wilaya katika Jimbo la Iowa ni lazima iwasilishe mpango wake kufikia Julai 1, wakielezea jinsi tutakavyoshughulikia tatizo la kukomeshwa kwa masomo lililosababishwa na shule kufungwa baada ya COVID- 19, na pia kutambua hatua muhimu kuhusiana na mahitaji ya mwanafunzi ya kijamii na kihisia, afya na usalama, kalenda zinazofafanua kwa kina pamoja na mipangilio, mahitaji ya kiteknolojia na jinsi ya kutekeleza masomo ya haraka.

Timu yetu ya shule za Davenport imekuwa ikiangazia hatua hizi muhimu ili kuunda Mpango wa Kurudi Masomoni ambao unahusisha uwezekano wa jinsi tatu: kusoma shuleni, kusoma kwenye mtamndao au kuchanganya masomo ya mtandao na yale ya shuleni.

Tafadhali tambua, usalama wa wanafunzi wetu, walimu, wafanyakazi na jamii ni wa umuhimu mkubwa kwetu wakati tunaamua jinsi masomo yataendelea katika mwaka wa masomo wa 2020-2021. Uamuzi wetu wa mwisho utategemea na hali katika jimbo kama itakavyoelekezwa na Gavana Reynolds, Idara ya Afya ya Umma ya Iowa, Vituo vya Udhhibiti wa Magonjwa na idara ya afya ya mtaa, ambayo tunakutana kila wiki.

Bila kujali njia ya kusoma ambayo itatumika, wanafunzi wote wa shule za Davenport

Community School District wataanza shule Jumatatu Agosti 24, 2020.

Tunajua kuwa utakuwa na maswali mengi kuhusu mpango wa kurudi shuleni, na jinsi Wilaya inavyoyatarisha majengo yake ikiwa masomo ya shuleni yatafanyika mnamo Agosti.

Katika wiki zijazo, utakuwa ukipokea taarifa muhimu ambazo zinayajibu mengi ya maswali yako na wasiwasi kuhusu Mpango wa Kurudi Masomoni, na mtoto wako kurudi shuleni.

Tunafanya kila jitihada kuhakikisha kuwa kila familia katika Davenport Community School District iko na vifaa na vitu vinavyohitajika kupokea taarifa hizi muhimu.

Kaa kwenye tovuti ya Wilaya, akanti za mitandao ya kijamii, na barua pepe yako kwa taarifa nyingi muhimu zitakazofuata ambazo zitaangazia maswali yako na kukupatia fursa ya kutoa maoni.

Tunatazamia kuanza shule tena mnamo Jumatatu, Agosti 24, 2020

Kuwa Salama!

